

**MAKATIBU WA AFYA NCHINI WATAKIWA KUWASILISHA
TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KIUTUMISHI
TUME YA UTUMISHI WA UMMA KWA WAKATI**

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.

Makatibu wa Afya katika Mikoa na Wilaya Tanzania Bara wametakiwa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za kiutumishi kwa wakati kila baada ya robo mwaka katika kipindi cha mwaka.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma, Bibi Thecla Shangali ameyasema hayo katika Mkutano wa kazi wa Idara ya Utumishi wa Afya unaomalizika leo katika Ukumbi wa Nyinda Classic Hotel Jijini Tanga.

Bibi Shangali ametaja lengo kubwa la kuwasilisha taarifa mbali mbali za kiutumishi ni kuwezesha Tume ya Utumishi wa Umma kuona na kulinganisha hali ya Utumishi na kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu usimamizi na maendeleo ya watumishi nchini.

Akiwasilisha mada kuhusu uwasilishaji wa taarifa Tume katika mkutano huo Bw. Mdoe Robert Mdoe Katibu Msaidizi katika Idara ya Utumishi wa Afya ameanisha taarifa zinazotakiwa kuwasilishwa Tume ya Utumishi wa Umma kuwa ni pamoja na taarifa za ajira, Kuthibitishwa kazini, Upandishwaji vyeo, Tange za watumishi, Mafunzo ya watumishi na masuala ya nidhamu.

Aidha Bw. Mdoe amezitaja taarifa nyingine zinazotakiwa kuwasilishwa Tume ya Utumishi wa Umma kuwa ni watumishi walioondolewa katika Utumishi wa Umma baada ya kushindwa kutimiza sifa za kiutendaji katika kipindi cha majaribio, watumishi waliopatikana na makosa ya kinidhamu, watumishi waliohamishwa kutoka kwa Mwajiri au Mamlaka husika kwenda nyingine, watumishi walio na kesi mahakamani na watumishi ambao rufaa zao zimeshughulikiwa na TSD Makao Makuu zilizokatwa dhidi ya Kamati za nidhamu za mikoa na taarifa za utekelezaji wa OPRAS.

Pamoja na uwasilishaji wa taarifa za kiutumishi kwa wakati, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma Bibi Shangali amezitaka

pia mamlaka katika sekta ya Afya kuhakikisha kuwa sekta ya Afya inapata watumishi wenye sifa kwa mujibu wa kanuni na taratibu za ajira zilizopo katika Utumishi wa Umma. Amefafanua kuwa sekta ya Afya ni sekta nyeti kwani inashughulikia afya za watu/uhai wa watu hivyo mamlaka zinazohusika na ajira zinapaswa kuwa makini na uangalifu wa hali ya juu.

Kuhusu suala la maadili katika Utumishi wa Umma, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma Bibi Shangali amewataka pia watumishi katika sekta ya Afya kuzingatia maadili katika uendeshaji wa shughuli zote za Utumishi wa Umma ili kutoa huduma bora kwa Watanzania.

Mkutano wa kazi wa Idara ya Utumishi wa Afya, ambao madhumuni yake yaliainishwa na Naibu Katibu wa Idara hiyo, Bw. Samuel Ngatunga kuwa ni kutathmini utekelezaji wa kazi za Makatibu wa Afya wa Mikoa na kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto za kazi hizo. Mkutano ulianza tarehe 10.02.2010 na unatarajiwa kufungwa leo saa 8:00 mchana.

Mkutano huo ulihusisha Makatibu wa Afya wa Mikoa, Majiji, Hospitali za Rufaa, Hospitali Maalum na Wadau mbali mbali wa Sekta ya Afya.

Iwapo una maoni/maswali, Tafadhali tuandikie:-

Katibu,
Ofisi ya Rais,
Tume ya Utumishi wa Umma,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.